



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE



Unapojibu Tafadhali taja:

Kumb Na: NTC/ TD/US/620/VOL1 A/71

12/08/2024

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA AJIRA YA MUDA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe anapenda kuwatangazia wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa, kuomba nafasi za muda kama ifuatavyo:-

MWALIMU WA MALEZI WA WATOTO WADOGO MCHANA- NAFASI 01

Sifa za Mwombaji

Awe na elimu kidato cha nne(Form four), au kidato cha Sita(Form Six), aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika fani ya malezi ya watoto wadogo mchana kutoka chuo kinachotambulika na serikali.

KAZI/MAJUKUMU

1. Kuwapatia watoto malezi bora, kuwapa mwongozo na mwenendo bora wa maisha, utii, heshima na ushirikiano.
2. Kutunza kumbukumbu zote na usimamizi wa kanuni za kituo cha kulelea watoto wadogo mchana.
3. Awe na uwezo wa kuzifahamu na kudhibiti tabia na mienendo mibaya kwa watoto.
4. Kuwapatia watoto huduma ya chakula wanapokuwa kituoni ili kukuza afya zao.
5. Kuwapatia watoto mazingira bora yanayoweza kukuza akili, mwili na hisia zao.
6. Awe na uwezo wa kuendeleza vipaji vya watoto na kuwaandaa kwa ajili ya kujiunga na shule za msingi.
7. Awe na uwezo wa kumudu matatizo yake binafsi ili yasiingilie utendaji wake wa kazi.

8. Kutambua maendeleo ya mtoto na kuweza kushauri Mzazi.
9. Kutunza mali za serikali na muda.
10. Asiwe na rekodi ya uhalifu na utelekezaji familia.
11. Kufanya kazi nyingine atakazo pangiwa na muajiri wake.

MSHAHARA

Kiwango cha mshahara kitategemea masharti ya mkataba.

MASHARTI YA WAOMBAJI

1. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania wenye umri usiozidi miaka 35.
2. Waombaji wote waambatanishe vyeti vya kuzaliwa.
3. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza(Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini(referees 3) wa kuaminika.
4. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma cheti cha kidato cha nne, na cheti cha kuhitimu mafunzo kwa walimu wa malezi.
5. Waombaji waambatanishe picha za passport size mbili (2) za hivi karibuni.

Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **30/08/2024** Siku ya Ijumaa saa tisa na nusu alasiri.

.....
K. Sadick

K. SADICK

MKURUGENZI

HALMASHAURI YA MJI NJOMBE



Ofisi ya Mkurugenzi (TD), S.L.P 577 NJOMBE, Tovuti: www.njombetc.go.tz, Simu: 026-2968833

Barua pepe: td@njombetc.go.tz, Posti Kodi : 31 Barabara ya Ikisa, 59108 Mjimwema -Njombe